

akiwasilisha ripoti ya utunzaji mazingira iliyotanywa na benki hiyo Dar es Salaam jamaa, wame... wa Kampuni ya Bia Serengeti (SBL), Mark Ocitti na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Refi Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa. (Picha na Rahel Pallangyo).

kweli.

* Mtaalamu asema homa ya nguruwe haina madhara kwa wanadamu *

Na Shukuru Mgoba, Mbeya

IMEELEZWA kuwa ugonjwa wa homa ya nguruwe hauna madhara yoyote kwa binadamu na kwamba hata ikiwa mtu amekula nyama ya nguruwe mwenye ugonjwa huo hapati athari yoyote.

Hayo yalibainishwa jana na Daktari wa Mifugo Mkoa wa Mbeya, Samora Mshani wakati alipozungumza na HabariLEO kuhusu zuio la

kusafirisha nguruwe kutoka eneo moja kwenda lingine kutokana na mlipuko wa homa ya nguruwe.

"Nguruwe ambaye ameumwa ugonjwa huu anakufa ndani ya kipindi kifupi, hata kukonda hakondi na nyama yake ni nzuri na inaweza ikaliwa na binadamu pasipo binadamu yeyote yule aliyekula nyama hiyo kuathirika, kwa sababu ugonjwa huo haumwambukizi binadamu," alisema Dk Mshani.

Alisema ugonjwa wa

homa ya nguruwe unaenezwa na virusi na hauna tiba na kwamba kinachowafanya wasisitize nguruwe aliyekufa na ugonjwa huo kutoliwa ni kwa sababu ya usafirishaji wa nyama hiyo kwenda eneo lingine unaweza kueneza ugonjwa huo kwa nguruwe wengine.

Alisema ili kudhibiti ugonjwa huo wafugaji wanapaswa kuwapa nguruwe chakula cha kutosha, kuzingatia usafi wa mabanda, kuhakikisha nguruwe wote wanafanyiwa ukaguzi

wa kitaalamu pamoja na kuhakikisha nguruwe waliopata ugonjwa wanafukiwa kwenye shimo refu au wanachomwa moto.

"Kama nilivyosema awali ugonjwa huu hauna tiba hivyo kuchukua tahadhari za mapema ili kudhibiti usiingie ndio jambo la msingi na sisi kwenye mikoja yetu ya Nyanda za Juu Kusini tulishaweka zuio la usafirishaji wa nguruwe muda mrefu hivyo wananchi wanapaswa kutopuuza hili agizo," alisema.

Aliiongeza kuwa ugonjwa huo upo nchini kwa muda mrefu lakini huzuka kwa kasi zaidi kipindi cha masika kwa sababu uwezekano wa kusambaa kwa sababu ya maji kuwa mengi ni mkubwa.

Aliwataka wananchi kutokuwa na hofu ya ulaji kitoweo hicho kwa sababu binadamu akila nyama ya nguruwe hapati ugonjwa wowote ule na kwamba wafugaji wanapaswa kuchukua tahadhari zinazotolewa ili kuepuka hasara.